

Maswali

1. Waisraeli walisafiri kwa muda gani jangwani?
2. Nani alikuwa kiongozi wao mpya baada ya Musa kufa?
3. Hema kubwa iliyojengwa na Musa iliitwaje?
4. Safina lilikuwa namna gani?
5. Nani aliishi katikati ya makerubi ya Safina?
6. Mungu aliambia Yoshua afanye nini walipofika Mto Yordani?
7. Nini ilifanyika makuhani walipokanyaga ndani ya maji?
8. Waisraeli walifanya nini wakati makuhani walikuwa wamesimama katikati ya mto.
9. Watu 12 walifanya nini?
10. Nini ilifanyika wakati makuhani waliganyaka kwa ukingo wa mto.

Majibu

1. Waisraeli walisafiri jangwani kwa muda wa miaka 40.
2. Yoshua ndiye alikuwa kiongozi mpya baada ya Musa kufa.
3. Hema kubwa iliitwa Maskani.
4. Safina ilikuwa sanduku kubwa iliyofunikwa na dhahabu na makerubi ya dhahabu kila pande.
5. Mungu aliishi katikati ya makerubi.
6. Lazima makuhani wabebe sanduku mpaka kando ya mto na wawe wa kwanza kuganyaka ndani ya maji.
7. Mto uliacha kuteremka na kukawa na njia kavu.
8. Waisraeli walivuka kwa njia kavu.
9. Watu 12 kila mmoja alichukua jiwe katikati ya mto na akapeleka kwa Nchi ya Ahadi na wakafanya kituta.
10. Makuhani walipoganyaka kwa ukingo wa mto, maji yalirudi na kuendelea.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



18 Kuvuka Mto wa Yordani

Marejeo

Yoshua 3:14 – 17 na 4:1 – 11

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu alitumia uwezo wake kupeleka watu wake mpaka Nchi ya Ahadi

Maneno maalum

- 18.1 Waisraeli + kiongozi mpya + Yoshua + Hema + Safina + Mungu alikuwa nao
- 18.2 Mto wa Yordani + pana sana + Mungu + Yoshua + kuhani + Safina + ukingo wa mto + njia kavu
- 18.3 Makuhani + katikati ya mto + watu + vuka mto + watu 12 + mawe + tuta + kumbusha + Mungu alisaidia
- 18.4 Vuka salama + makuhani + Nchi ya Ahadi + mto ulirudi + watu walifurahi + shukuru Mungu

18.1 Waisraeli walizunguka zunguka jangwani kwa miaka 40. Baadaye waliona kwa umbali vilima vya Nchi ya Ahadi ng'ambo ya Mto mkuu wa Yordani. Walijua kwamba walikuwa wanakaribia mwisho wa safari yao.

Musa, kiongozi wao mkuu, alikufa kabla ya kufika Nchi ya Ahadi. Mungu aliwapa kiongozi mwigine kuwapeleka kwa nchi yao. Kiongozi mpya aliitwa Yoshua.

Wakati walikuwa wakisafiri jangwani, Mungu aliambia Musa atengeneze hema kubwa iliyoitwa Maskani. Pale ndipo watu walikuja kuabudia Mungu. Ndani, katikati ya Maskani kulikuwa na chumba ndogo iliyoitwa Patakatifu Sana. Kuhani Mkuu pekee yake aliruhusiwa kuingia kwa kile kichumba. Pale Patakatifu Sana kulikuwa na Sanduku. Hili lilikuwa sanduku lililofunikwa na dhahabu tupu. Ndani ya Sanduku kulikuwa na vipande viwili vya mawe yenye Mungu aliandika sheria zake. Kando ya kila upande wa Sanduku, kerubi ilisimama, mfano wa malaika. Ziliundwa kwa dhahabu tupu na mabawa zake zilifunika juu ya Sanduku. Mungu alikaa ndani ya makerubi juu ya Sanduku, kwa hivyo alikuwa na watu wakati wote.

Sanduku lilikuwa la maana sana kwa sababu ndipo Mungu aliishi ili awasaidie Waisraeli kila mara. Sanduku lilikuwa la maana na takatifu kwa sababu utukufu wa Mungu ulikuwa katikati ya makerubi. Hakuna aliyeruhusiwa kuligusa lile Sanduku la sivyo angekufa. Makuhani wangebeba lile Sanduku kwa nguzo mbili. Wakati Waisraeli walitembea na Sanduku, walijua Mungu ako nao.

18.2 Mwishowe Waisraeli walifika ukingo wa Mto wa Yordani. Pale wangeona Nchi ya Ahadi upande mwingine wa mto. Kwa siku tatu walipiga kambi kando ya Mto Yordani. Mto ulikuwa pana sana na walishindwa vile wangeweza kuvuka mpaka ng'ambo. Mungu alinena na Yoshua na kumwambia kwamba lazima makuhani wabebe Sanduku mpaka ndani ya mto ili waweze kuvuka ng'ambo.

Yoshua hakujua vile hii itasaidia lakini kwa sababu aliamini Mungu, alifanya vile Mungu alisema. Makuhani walibeba Sanduku. Waliganyaka kwa maji kando ya mto. Maji yalisimama kwenda na kukawa na njia kavu mtoni.



18.3 Makuhani wakibeba Sanduku walitembea mpaka katikati ya mto na wakasimama. Watu wote walitembea kwa njia kavu. Kisha wote walifika ng'ambo ingine. Yoshua aliambia watu kumi na wawili wabebe kila mtu jiwe moja kubwa kutoka chini katikati ya mto. Walipovuka walitengeneza kituta cha mawe kando ya mto katika Nchi ya Ahadi.

Kituta cha hayo mawe kilikaa hapo kwa miaka mingi. Hicho kituta cha mawe kiliwakumbusha vile Mungu aliwasaidia kuvuka huo mto. Mungu aliwaleta mpaka kwa Nchi ya Ahadi.

18.4 Baada ya kila mtu kuvuka mto, makuhani walibeba Sanduku kutoka katikati ya mto mpaka kwa Nchi ya Ahadi. Makuhani walipoganyaka kwa ukingo wa mto kwa Nchi ya Ahadi, maji yalirudi na kuendelea. Ilikuwa nguvu ya Mungu katikati ya makerubi iliyokuwa kwa Sanduku ndiyo ilishika maji ili watu wote wavuke.

Watu walifurahi kwa sababu mwishowe walikuwa wamefika salama kwa Nchi ya Ahadi. Walishukuru Mungu sana.